Recent

Photo

# SUJI SECONDARY SCHOOL

Operated by

**NORTH EAST TANZANIA CONFERENCE OF THE SEVENTH DAY ADVENTIST CHURCH**

P. O. BOX 351, Same – Kilimanjaro Cell: **+255765434991/0756779195/0714574426**

Tovuti: www.sujisec.ac.tz. *Barua pepe:* info@sujisec.ac.tz.

---

## MAOMBI YA KUJIUNGA NA SHULE KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2024

SUJI ni shule ya sekondari inayoendeshwa kwa falsafa ya elimu ya kanisa la Waadventista Wa Sabato kwa kufuata kanuni, taratibu na miongozo ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Ni shule inayojitoa kikamilifu katika kulea vyema na kukuza watoto wetu kiakili, kiroho, kimwili na kijamii. Shule inapatikana katika mazingira mazuri na tulivu yenye walimu bora wenye juhudi za kufundisha kwa umahili.

**MAHALI SHULE ILIPO**

Shule ipo katika Mkoa wa Kilimanjaro, Wilaya ya Same, Kijiji cha Malindi – Suji.
Unaposafiri kwa mabasi yanayotoka Tanga/DSM/Morogoro kwenda Moshi/Arusha, teremka Makanya. Makanya ni kituo kabla ya kufika Same mjini ukiwa unatokea Dar es salaam. Kwa mabasi yanayotoka Arusha/Moshi kwenda Tanga /Morogoro Makanya ni kituo baada ya Same mjini.

### A. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

- Bandika picha ya hivi karibuni ya mtoto (passport size) kwenye kisanduku hapo juu.
- Lugha ya mawasiliano na kufundishia ni Kiingereza.

### B. SEHEMU HII IJAZWE NA MWOMBAJI KWA HERUFI KUBWA

1. Jina la Mwanafunzi …………………………………………………………………………….
2. Tarehe ya kuzaliwa …………………………………………………………………………
3. Shule uliyomalizia darasa la saba ………………………………………………………………..
4. Anuani ya kudumu ………………….Namba ya Simu ya mzazi/mlezi…………………….
5. Je, unalo tatizo la kiafya? (Taja) ……………………(Ambatanisha na vielelezo vya daktari)
6. Dhehebu lako ……………………………………………………………………………...

### C. USHUHUDA WA MWANAFUNZI

Mimi …………………............................... (Jina la mwanafunzi) endapo nitachaguliwa kuwa mwanafunzi wa shule hii, nitakubali na ninaahidi kushirikiana na uongozi wa shule kufuata kanuni na miongozo ya kanisa la Waadventista Wa Sabato na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia.

Sahihi ………………………………………

**D. SEHEMU HII IJAZWE NA MZAZI/MLEZI**

1. Jina kamili ………………………………………… Mzazi/Mlezi …………………………….
2. Kazi yako ………………………………………………………………………………..
3. Anuani yako ya kudumu (sanduku la posta) na namba ya simu ………………………….
4. Tarehe …………………………………………………………………………………….

**E. USHUHUDA WA MZAZI**

Ikiwa mwanangu atachaguliwa kuwa mwanafunzi wa shule hii, ninaahidi kushirikiana na uongozi wa shule kufuata kanuni na miongozo ya kanisa la Waadventista Wa Sabato na Wizara ya Elimu, sayansi na Teknolojia. Aidha ninaahidi kulipa ada ya shule kwa uaminifu na kwa wakati.
Sahihi …………………………………………….

**F. UTARATIBU WA MALIPO YA ADA YA SHULE (UKURASA WA SITA (6)**

(a) Ada na malipo mengine ya shule yatafanyika kupitia akaunti za benki tu na si vinginevyo. Akaunti zetu za benki ni **NMB Na. 40503500068** na **CRDB Na. 0150447102400** Jina ni Suji Secondary School. Tafadhali andika jina la Mwanafunzi na kidato anachosoma kwenye "pay – in – slip" unapofanya malipo benki.

(b) Mpatie mwanao hati halisi (Original pay – in-slip) ya malipo uliyofanya aje nayo wakati wa kufungua shule ili kuepusha usumbufu unaoweza kumfanya mwanafunzi asipokelewe shuleni. (Angalia kiambatanishi No 01).

**G. VIFAA NA MAHITATJI MUHIMU**

Mwanafunzi atapaswa kuja na vifaa vifuatavyo siku ya kuripoti au anaweza kuvipata shuleni kwa gharama iliyooneshwa kwenye jedwali hapa chini.

| S/N | AINA YA VIFAA | GHARAMA |
|---|---|---|
| 1. | Ndoo ya lita 10 | 5,000 |
| 2. | Godoro la sponji futi 3 | 50,000 |
| 3. | Blanket (nyeusi au blue) (Nzito) | Aje nayo |
| 4. | Vyombo vya chakula | 5,000 |
| 5. | Taulo | 10,000 au aje nayo |
| 6. | Madaftari, kalamu, vitabu vya masomo husika | |
| 7. | Dictionary ya kiingereza | Aje nayo |
| 8. | Mathematical set | 5,000 |
| | | |

Mwanafunzi anapaswa kuja na nguo zifuatazo:

| S/N | WAVULANA | WASICHANA |
|---|---|---|
| 1. | Suti nyeusi. Surual iwe na mifuko mitatu na isiwe ya kubana kabisa. | Sketi 1 rangi nyeusi na nyingine rangi ya Dark blue zishonwe mtindo wa rinda box ziwe ndefu zinazovuka magoti hadi chini usawa wa kiwiko cha mguu. |
| 2. | Suruali 1 rangi ya dark blue. Iwe na mifuko mitatu (3) (1 nyuma, miwili (2) mbele. | Koti jeusi (suit material). |
| 3. | Shati mbili nyeupe mikono mirefu (tetroni) | 'Track suit' nyekundu ya michezo (isiyo na maandishi). |
| 4. | Track suit'nyeusi ya michezo (isiyokuwa na | T-shirt ya njano 1 na nyeupe I (yenye |

| | | |
|---|---|---|
| | maandishi). | kola) |
| 5. | T-shirt ya njano 1na nyeupe 1 (yenye kola) | Jaketi moja jeusi lisilo na kofia kwa ajili ya baridi. |
| 6. | Jaketi moja jeusi lisilo na kofia kwa ajili ya baridi. | Soksi ndefu (stockings) nyeupe jozi 2. |
| 7. | Jozi 2 za viatu vya ngozi rangi nyeusi vyenye kisigino kifupi, vya kufunga kwa kamba na soksi nyeusi. | Jozi 2 za viatu vya ngozi rangi vyenye kisigino kifupi, vya kufunga kwa kamba. |
| 8. | Shuka jozi 2 rangi ‘blue’. | Shuka jozi 2 rangi ya ‘pink’ |
| 9. | Tai nyeusi mbili. | |

Siku ya kuripoti shuleni mwanafunzi aje akiwa amevaa sare zifuatazo:

- Wavulana: Suruali ya Dark Blue na T-shirt rangi nyeupe yenye kola.
- Wasichana: Sketi ya Dark Blue na T-shirt rangi nyeupe yenye kola.

Sare (uniform) zifuatazo zinatolewa hapa shuleni

- Wasichana – Sketi 2, Sweta 1, na T-shirt 2.
- Wavulana – Suruali 2, T-shirt 2, na Sweta 1.
- N.B Hakuna nguo nyingine zitakazoruhusiwa kuvaliwa hapa shuleni tofauti na zilizotajwa hapo juu.

## H. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Mwanafunzi akifika shuleni atapewa kijitabu cha sheria na taratibu zote za shule ni (STUDENT’S HAND BOOK).

Aidha mwanafunzi awapo shuleni azingatie haya.

1. Hairuhusiwi mwanafunzi kutumia lugha ya dhihaka au kejeli.
2. Lugha pekee rasmi itakayotumika shuleni ni lugha ya kiingereza.
3. Ni marufuku kwa mwanafunzi yeyote kutoshiriki katika shughuli yoyote ya shule bila kibali cha maandishi toka kwa mwalimu au idara husika.
4. Mwanafunzi hatoruhusiwa kutembelewa na mzazi/mlezi kinyume na tarehe iliyopangwa na shule isipokuwa kwa idhini maalumu kutoka kwa uongozi wa shule.
5. Ni marufuku kuendesha/kushiriki katika ushabiki wowote wa kisiasa.
6. Ni marufuku mwanafunzi kutumia vipodozi na aina yoyote ile ya dawa za kubadili rangi ya ngozi.
7. Ni marufuku kupiga kelele/mayowe katika eneo la shule isipokuwa katika mazingira maalumu kama uwanjani wakati wa michezo.
8. Mwanafuzi yeyote anao wajibu wa kutunza na kulinda mali zote za shule.
9. Mgeni yoyote haruhusiwi kuingia bwenini tafadhali zingatia.
10. Ni marufuku mwanafunzi kuingia bweni la jinsia tofauti na yeye.
11. Ni marufuku kufanya tendo lolote la jinai ndani na nje ya shule.
12. Mzazi/mlezi au wawakilishi watakao tembelea wanafunzi ni wale walioambatanisha picha zao kwenye fomu ya usajili, wakiwa wamevaa kwa staha.
13. Hairuhusiwi mwanafunzi kutumia simu ya mwalimu au mfanyakazi bila kibali kutoka kwa uongozi.
14. Hairuhusiwi kulala nje ya shule bila ruhusa ya Mkuu wa Shule.

15. Kukwepa masomo au mitihani na kutohudhuria vipindi bila ruhusa ya mwalimu wa somo au wa zamu.
16. Hairuhusiwi udanganyifu wowote katika mitihani hapa shuleni.
17. Hairuhusiwi kuchelewa shule bila sababu za msingi.
18. Hairuhusiwi kumiliki Simu, Radio, Camera na vitu vyote vya aina hiyo.
19. Hairuhusiwi kukwepa IBADA zote endesha hapa shuleni.

**MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI AFUKUZWE SHULE**

1. Wizi/Ujambazi.
2. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.
3. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi au jamii kwa ujumla.
4. Kupigana na mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.
5. Kufuga ndevu.
6. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
7. Uvutaji wa sigara.
8. Uasherati, mahusiano ya jinsia moja, kuoa au kuolewa.
9. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.
10. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule na kumiliki vifaa vya simu.
11. Uharibifu wa mali ya shule/mwenzako kwa makusudi.
12. Kudharau bendera ya Taifa na wimbo wa Taifa.
13. Kusababisha mimba au kupewa mimba.
14. Kugoma au kuendesha aina yoyote ya mgomo ndani/nje ya shule.
15. Kutohudhuria IBADA endeshwa hapa shuleni.

**ANGALIZO**

Simu hairuhusiwi shuleni, ni kosa la kufukuzwa shule iwapo mwanafunzi atatumia simu ya mwalimu au mfanyakazi mwingine bila kibali toka kwa uongozi mawasiliano yote yafanyike kupitia **SIMU NO**. **0718704553** au **0684558313** namba za Matron na **0785233399** namba za Patron.

**ORODHA YA VITABU VINAVYOTUMIKA SHULENI NI VYA TET**

(Taasisi ya Elimu Tanzania) kwa vidato vyote mpatie mwanao angalau vitabu vya masomo matano, Hesabu na English ikiwemo.

**MAHITAJI MENGINE**

**VITU VIFUATAVYO NI LAZIMA KUWANAVYO SIKU YA KURIPOTI SHULENI**

- Daftari (counter book 10-quire 3) na daftari za mazoezi 10 (msomi).
- Kalamu 10 na penseli 5.
- Sabuni 4 za kuogea zenye dawa.
- Vitabu walau vitano (5) vya masomo mbalimbali atakavyo vitunza mwanafunzi mwenyewe.
- Graph pad.
- Viatu vyeusi pair mbili kisigino kifupi vyenye kamba.
- Taulo ya kuogea.
- Dawa ya meno na miswaki.
- Kiwi na brashi
- Kitana

- Sandals (ndala aina ya bata/umoja) pair 02.
- Kata kucha
- Mafuta ya mgando ya kupaka Vaseline, Samona na movit
- Sahani na kikombe
- Pad kwa wasichana (Taulo za kike wasichana).
- Blanket 1.
- Vifaa vya michezo (raba na bukta), wavulana bukta rangi ya njano, wasichana Bukta nyeusi sketi za rangi ya njano za kuzungusha.

**NB:** Suji Sekondari ni shule inayoendeshwa na kumilikiwa na Kanisa la Waadventista Wa-sabato, Hivyo mwanao awapo hapa shuleni atafuata pia taratibu na miongozo ya kanisa pasipo kukengeuka. Hata hivyo linakuomba kumsisitizia mwanao bidii katika masomo ya kumpa sapoti katika mahitaji yake yatakayompelekea kufikia njozi yake.

Shule itafunguliwa tarehe **08/01/2024**.

SUJI SECONDARY SCHOOL
HEADMASTER
10 AUG 2023
P.O. BOX 351 SAME

JOSHUA S. OKELLO
**MKUU WA SHULE.**

**KIAMBATANISHO No 1**

## SEVENTH DAY ADVENTIST CHURCH
## NORTH EAST TANZANIA CONFERENCE (NETC)
## SUJI HIGH SCHOOL

### VIWANGO VYA ADA KIDATO CHA KWANZA HADI KIDATO CHA NNE (O – LEVEL)
### MWAKA WA MASOMO 2024

| | BWENI | KUTWA |
|---|---|---|
| **KIDATO CHA KWANZA** | 1,962,000.00 | 1,418,000.00 |
| **KIDATO CHA PILI** | 1,892,000.00 | 1,348,000.00 |
| **KIDATO CHA TATU** | 1,842,000.00 | 1,298,000.00 |
| **KIDATO CHA NNE** | 1,932,000.00 | 1,388,000.00 |

### MALIPO YANAFANYIKA KWA AWAMU NNE

| WANAFUNZI WA BWENI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **JANUARY** | **APRIL** | **JULY** | **SEPTMBER** |
| **KIDATO CHA KWANZA** | 762,000.00 | 350,000.00 | 600,000.00 | 250,000.00 |
| **KIDATO CHA PILI** | 692,000.00 | 350,000.00 | 600,000.00 | 250,000.00 |
| **KIDATO CHA TATU** | 642,000.00 | 350,000.00 | 600,000.00 | 250,000.00 |
| **KIDATO CHA NNE** | 732,000.00 | 350,000.00 | 600,000.00 | 250,000.00 |

| WANAFUNZI WA KUTWA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **JANUARY** | **APRIL** | **JULY** | **SEPTEMBER** |
| **KIDATO CHA KWANZA** | 518,000.00 | 300,000.00 | 400,000.00 | 200,000.00 |
| **KIDATO CHA PILI** | 448,000.00 | 300,000.00 | 400,000.00 | 200,000.00 |
| **KIDATO CHA TATU** | 398,000.00 | 300,000.00 | 400,000.00 | 200,000.00 |
| **KIDATO CHA NNE** | 488,000.00 | 300,000.00 | 400,000.00 | 200,000.00 |

SUJI SECONDARY SCHOOL
HEADMASTER
10 AUG 2023
P.O. BOX 351 SAME

JOSHUA S. OKELLO
**MKUU WA SHULE.**

# SEVENTH DAY ADVENTIST CHURCH
# SUJI SECONDARY SCHOOL

## MEDICAL EXAMINATION FORM – 2024

### KIAMBATANISHO No 2

To be completed by a medical officer in respect of all one(s) new entrants

Full name ________________________________________ age _________ sex__________________

Blood count (red and white ___________________________________________________________

Stool examination ___________________________________________________________________

Urine analyses ______________________________________________________________________

Skin _______________________________________________________________________________

Eyes _______________________________________________________________________________

Ears _______________________________________________________________________________

Syphilis test ________________________________________________________________________

T.B test ____________________________________________________________________________

Any disabilities ______________________________________________________________________

Spleen _____________________________________________________________________________

**ADDITIONAL INFORMATION** eg. Physical detects or impairment infections, chronic of family.

_________________________________________________________________________________

From the results shown above, I certify that the above student/pupil is fit unfit to pursue studies.

Signature ___________________________________________________________________________

Designation ________________________________________________________________________

Station ______________________________________________________________________________

Date ________________________________________________________________________________